

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA



MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI TASAF III

**TAARIFA FUPI YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MPANGO WA
KUNUSURU KAYA MASKINI KWA AWAMU KUMI KUENZIA
JULAI 2015, HADI JANUARI 2017**

**TAARIFA HII ITAHUSU UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MPANGO WA KUNUSURU
KAYA MASKINI TASAF AWAMU YA TATU
KUANZIA JULAI, 2015 HADI JANUARI, 2017**

1.0 UTANGULIZI

Uzinduzi wa TASAF awamu ya tatu, ulifanyika tarehe 07/10/2014 Wilayani Muheza katika ukumbi wa TARECU. Uliambatana na warsha ya siku moja ambayo iliratibiwa na kuendeshwa na viongozi kutoka TASAF makao makuu pia ilihudhuriwa na viongozi kutoka Wilayani wakiwemo Waheshimiwa Madiwani, viongozi wa dini, viongozi wa vyama. Wakuu wa idara na wawezeshaji wa wilaya walioteuliwa kwaajili ya utekelezaji wa zoezi la utambuzi na uhakiki wa kaya maskini. Mgeni rasmi alikuwa Mh. Mkuu wa Wilaya ambaye alimuwakilisha Mkuu wa Mkoa.

1.1 MALENGO YA TASAF AWAMU YA TATU

TASAF awamu ya tatu ni mpango wa kuwezesha kaya maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharimia mahitaji muhimu kwa kutoa ruzuku ya msingi naya masharti pamoja na huduma za elimu na afya.

- a) Ruzuku ya Msingi inatolewa kwa kila kaya iliyoandikishwa kwenye mpango ili kugharimia mahitaji ya msingi.
- b) Ruzuku ya masharti inatolewa kwa kaya zilizoandikishwa kwenye mpango zenye watoto wenye umri wa kwenda shule na kliniki kwa masharti ya kuhudhuria shuleni na clinic kwa kiwango kinachokubalika na mpango.

Ndani ya mpango huu, kaya maskini zinanufaika kwa kushiriki katika mpango wa Jamii wa uhawilishaji Fedha (Utoaji wa fedha), Mpango wa Miradi ya Ujenzi ambayo itatoa fursa za ajira za muda katika kipindi cha hari, shughuli za kuweka akiba pamoja na kuwekeza katika shughuli za kuongeza kipato na kujengewa uwezo. Jumla ya walengwa 7591, wameandikishwa kwenye mpango katika vijiji 90 vilivyoko kwenye mpango kati ya Vijiji 135 vya Wilaya ya Muheza. (taarifa kamili ziko kwenye fail na computa kwaajili ya kusoma zaidi).

Hadi sasa tunatekeleza lengo moja tu la uhawilishaji fedha Vijijini (utoaji fedha vijijini) wakati tukisubiri maelekezo toka TMU ya kuendelea na malengo mengine.

2.0 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MPANGO

2.1 SHUGHULI ZA UHAWILISHAJI FEDHA

katika kipindi cha Julai,2015 hadi Disemba,2016 shughuli zilizofanyika ni za uhawilishaji wa fedha kwa Kaya maskini ambazo zilifanyika kwa awamu kumi.

Shughuli hizi zilifanyika kwa ushirikiano wa wawezeshaji toka Wilayani wajumbe wa kamati za vijiji (CMC) viongozi wa Vijiji, Kata na Wilaya.



Walengwa wakiwa wanapata elimu kutoka kwa wawezeshaji matumizi sahihi ya ruzuku wanayopewa katika kijiji cha Kilulu

2. 1.1 MAFUNZO

Kabla ya kuanza shughuli za uhawilishaji fedha kwa Kaya maskini wawezeshaji 53 akiwemo mratibu na mhasibu wa Wilaya walipatiwa mafunzo ya uwezeshaji vijijini na baada ya hapo walienda kuwezesha pia wajumbe wa kamati za vijiji ambao wamechaguliwa kwa kila kijiji wajumbe 14 waliwapatia mafunzo yaliyowawezesha kuelewa na kufuata taratibu zote za mpango kama ilivyokusudiwa kutekelezwa katika nchi nzima. Wajumbe hawa ndio wanaohusika na usimamizi wa malipo kwa walengwa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa walengwa wakiwa chini ya usimamizi wa Wawezeshaji wa Wilaya. Pia waalimu wa shule za Sekondari, Msingi, Waganga na manesi wa shule na vituo ambavyo watoto wa walengwa wanasoma walipatiwa mafunzo ya uelewa wa mpango wa TASAF awamu ya tatu na jinsi ya kujaza fomu za elimu na afya.

3.1 SHUGHULI ZILIZOFANYIKA VIJIJINI.

Wawezeshaji wa wilaya hupangiwa kwenda kusimamia shughuli za uhawilishaji fedha kwenye vijiji 90 vilivyoko kwenye mpango, shughuli kubwa wanayokwenda kuifanya ni kutoa mafunzo kwa wanakamati kila mmoja na wajibu wake (CMC), kwa kila kijiji wako CMC 14 hivyo huwa kila wakati wa malipo wanapeana zamu (7,7).

Wawezeshaji wanatangulia siku moja kabla, au kama ni vijiji vya karibu wanakwenda asubuhi sana kutoa elimu ya matumizi sahihi ya fedha zinazotolewa kwa kuanzisha miradi midogo midogo ikiwemo ya ufugaji wa kuku, kuunda vikundi vya kuweka na kukopa, kuboresha makazi, kuwasimamia watoto wahudhuri shuleni pamoja na kliniki.

Pia walengwa na wanakamati wa kusimamia shughuli zote za fedha vijijini (CMC) pamoja na kusimamia zoezi zima na kuhakikisha fedha zinawafikia walengwa waliokusudiwa kwa usahihi kama ilivyopangwa. Kabla ya kuanza malipo tunafanya kikao cha siku moja kwaajili ya maandalizi na kuelekezana mambo yote yanayotakiwa kwenda kufanyika vijijini, pia ni wakati muafaka wa kushirikishana changamoto wanazokutana nazo vijijini na kujadili jinsi ya kuzitatua. Baada ya hapo wawezeshaji wanasomewa ratiba na kujiandaa kwenda vijijini.



Ukarabati wa makazi ya nyumba kwa kaya lengwa kijiji cha Kisiwani

4.0 MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA

4.1 MAPATO:

Hadi kufikia mwezi Januari, 2017 tumeweza kupokea jumla ya Tshs. **2,746,278,000** sawa na asilimia 99% ambazo kati ya fedha hizo Tshs. **2,447,252,364** sawa na asilimia 88% ni fedha za walengwa pamoja na Tshs. **41,610,273** sawa na asilimia 1.5% fedha za uendeshaji Vijijini na Tshs. **235,791,545** sawa na asilimia 8.5% ni fedha za uendeshaji Wilayani, na Tshs. **27,740,182** sawa na asilimia 1% fedha za uendeshaji kwa maafisa ugani wanaokwenda kwenye Kata, ila kwakuwa 1.5% ya Vijiji huwa haitoshi inabidi kujazia kwa kila kijiji kupata walau Tshs. 70,000/-. Fedha hizi zilipokelewa katika wilaya ya Muheza toka TASAF Makao Makuu kwa

ajili ya utekelezaji wa zoezi la uhawilishaji fedha kwa kaya maskini katika vijiji 90 vilivyoteuliwa kuingia kwenye Mpango kati ya vijiji 135 vyenye kaya 7,591 zilizopitishwa kwenye mikutano mikuu ya Vijiji kama mwongozo wa TASAF ulivyoelekeza.

4.1.2 MATUMIZI

Jumla ya matumizi yalikuwa kiasi cha Tshs. **2,746,278,000/=** na fedha iliyobaki ni Tshs. **47,068,000/-** ambayo ni ya walengwa waliofariki, kuhama, Viongozi waliotolewa na wengine hawakuwepo fedha zote zimerudishwa TASAF Makao Makuu kutokana na walengwa kufariki, kuhama, kusafiri kwa kipindi, viongozi hasa wajumbe wa Serikali za vijiji.

5.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITokeza WAKATI WA UTEKELEZAJI.

Zipo changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji shughuli za uhawilishaji fedha kama ifuatavyo:-

- Hadi sasa jamii inaelewa kuwa mpango unalenga maskini mmoja mmoja na sio kaya maskini mfano, Wajane, Yatima na Wazee n.k..
- Ushiriki mdogo wa wananchi kwenye mikutano hasa mikutano mikuu ya vijiji ambayo imepelekea watu wengi kuja ofisi ya TASAF Wilaya kuomba kuingizwa kwenye mpango.
- Malipo ya fedha kwa kila awamu kuanzia Julai hadi Januari kupungua na kusababisha uendeshaji wa mpango kuwa mgumu hasa matumizi ya 1.5% za Vijiji na 8.5% za Wilaya.
- Hadi sasa kuna tatizo la kutambua uhalisia wa majina ya watoto wanaosoma shule za msingi, sekondari na wanaokwenda kliniki sababu kubwa ni wazazi wengine kuandikisha majina ya watoto kwenye mpango ambayo ni tofauti na yalioandikwa shuleni au kliniki.

6.0 UTATUZI WA CHANGAMOTO

- Kuendelea kuhamasisha jamii kwa njia ya kutumia vyombo vya habari, madiwani, viongozi wa serikali na wadau wengine wa maendeleo ili waweze kuelewa kwa kina juu ya mpango huu wa kuondosha dhana potofu miongoni mwa jamii kwamba mpango unalenga kaya maskini zaidi na sio maskini mmoja mmoja, walemavu na wazee.
- Maandalizi yafanywe mapema ya kutoa taarifa kwa walengwa ili waweze wote kuhudhuria mikutano na chaguzi ziwe za halali.
- Walengwa waelimishwe kupeleka watoto wao shuleni na kliniki ili fedha zisipungue pia kuhakikisha wanaandikisha majina ya watoto ambayo ni sahihi.

7.0 MAFANIKIO

Uhawilishaji wa fedha kwa njia ya kupokea ruzuku umeweza kuwanufaisha walengwa kwa kuboresha makazi yao, kuongeza mahudhurio shuleni, kuwa na uhakika wa kupata matibabu pindi wakiugua kwa kujiunga na CHF, watoto chini ya miaka mitano kupelekwa kliniki kwa wakati na kujiunga kwenye vikundi vya kuweka akiba na kukopa (VICOBA). Ingawa kuna changamoto kubwa ya walengwa ambao hawastahili waliotolewa kwenye mpango, ambao baadhi yao ni viongozi wa vijiji na wale waliotolewa kwenye mikutano mikuu ya vijiji kwamba hawastahili ili hali waliwaingiza kwamba wanastahili.



*Elizabeth akiwa kwenye Bustani ya mbogamboga
Kijiji cha Majengo*



*Mwajuma aliyeweza kufyatua tofali
Kijiji cha Mafere*

THIS INFORMATION WILL INCLUDE THE IMPLEMENTATION OF THE RESCUE PLAN ACTIVITIES FOR POOR HOUSEHOLDS TASAF III FROM JULY 2015 TO JANUARY 2017

INTRODUCTION

TASAF launch of third phase took place On 7 July, 2014 Muheza District in TARECU Hall. Coincided with the one day workshop, coordinated and operated by officials from the district among them councilors, religious leaders, leaders of the parties, Head of department and district facilitators chosen for implementation of exercise of verification of poor households. Guest was Honorable District Commissioner who represents Regional Commissioner.

1.1 GOALS OF TASAF PHASE THREE

TASAF phase three is an initiative to empower poor household's to increase income opportunities and the ability (payment of the requirements for subsidizing basic and attached with educational services and health.

Basic grants are provided to all households registered on the program to cover the needs of basic conditions.

Grants provided for in the plan which registered household containing children of school and clinics in terms of attendance at school and clinic at rate agreed with programme. Within this programme, poor households benefit by participating in social money transfer programme. The plan of construction projects that will provide temporary employment opportunities during the summer, with the activities of savings and invest in income generating activities and capacity building. The total of 7, 591 beneficiaries have enrolled in the program 90 villages existing in the programme among 135 villages of the district of Muheza.

So far, we perform only one goal of transfer of rural financial) provision rural finance) while we waited for instruction from TMU to proceed with other goals.

2.0 IMPLEMENTATION OF ACTIVITY OPLAN

2.1.1 INITIATIVES OF FUND TRANSFER

In the period of July 2015 to January 2017 activities undertaken are funds transfer to poor households that took place in window 1 up to window 10. These activities were conducted with the cooperation of facilitators from the district, members of village committees (cmc's), village leaders, ward and district.



Beneficiaries listened instructions of proper use of funds paid from the facilitators at Kilulu village

2.1.1 TRAINING

Pre-activity funds transfer to poor households facilitators 53, including the coordinator, and accountant of district were trained in facilitation rural and thereafter the may open to the villages members 14 undergone training that help them to understand and follow all procedure as implemented in whole country. This members are responsible for the management and beneficiaries including providing education for beneficiary while under supervision of secondary schools, primary, physicians and nurses of schools and centers that target studied were trained in understanding design of phase TASAF III how to fill the forms of Education and Health.

3.1 ACTIVITIES CONDUCTED IN RURAL

Facilitators of the district are scheduled to supervise the activities of funds transfer to the villages 90 bodies in the programme. A great activity they are going to do is provide training in each village are CMC's it is always charging the turns.

Facilitators are gone the day before or the nearby villages going very morning providing the proper use of funds provided to establish small projects including the proper use of funds provided to establish small business including poultry, create saving and credit groups, improved housing, supervise children attend schools with clinics.

Also targeted by the committee to look after all financial transactions in rural areas (CMC's) in addition to managing the whole process and ensure the money reaches the target audience for accuracy as planned. Before starting the session we will charge one day for preparation and rivalry done everything required to rural also an opportune time to share the challenges they faced in

rural areas and to discuss how to solve them. Thereafter, facilitators rehearsed schedule and prepare to go to rural areas.



Renovation of households of beneficiaries at Kisiwani village

4.0 REVENUE AND EXPENDITURE OF FUNDS RECEIVED FROM TASAF MANAGEMENT UNIT (TMU)

4.1 REVENUE (INCOME)

By January 2017 we have received a total **Tshs. 2, 746,278,000/=** equivalent to 99% of the funds that between **Tshs. 2447, 252,364/=** equivalent to 88% of the funds are targeted with **Tshs. 41,610,273/=** equivalent to 1.5% of operating at rural level and **Tshs. 235,791,545/=** equivalent 8.5% is cash operating district level and **27,740,182/=** equivalent to 1% cash operating extension officers who go to the country except that 1.5% of the villages are not enough we have to compensate for all the villagers to get at least Tshs. 70,000/= Those funds were received in Muheza from TASAF Headquarter for the implementation of the exercise of the transfer funds to poor households based in villages in 90 villages selected to enter into a programme containing households 7,591 adopted at the general meetings of villagers as guides TASAF directing.

4.1.2 EXPENDITURE

Total consumption grew amount of **Tshs. 2,746,278,000/=** and the remaining money is Tshs. **47,068,000/=** which is targeted deceased migrate. Leaders drawn and others were not present all the money has been returned to TASAF headquarter due to the beneficiary's death, shift travel for the period, heading mainly members of the village governments.

5.0 CHALLENGES FACED DURING IMPLEMENTATION

There are various challenges uncouncted when implementation funds transfer operation as follow:

So far the community understands that the programme focuses on individual poor and not poor households example widows, orphans, the elderly etc.

1. Participation of community members in meeting especially village assemblies which led people to come spleen TASAF office requesting inclusion in the programme.
2. Cash payments for each phase from July to January decline resulting in operational planning especially difficult spending 1.5% of wards to 8.5% of the district
3. So far, no problem recognizing the reality of the names of children attending primary school, secondary school and attending the clinic is the main reason parents enroll children in the programme names that are different from the written schools or clinic.

6.0 SOLVING THE CHALLENGES

1. Continue to encourage community by using media, councilors, government officials and other development partners in order to know in detail about this programme, removing the wrong notions among the communities that faces on poor households and not individually disabled and the elderly.
2. Preparation should be made in advance to provide information to beneficiaries so that they can attend the meeting and elections as legitimate
3. Beneficiaries should be instructed to fund their children to school their children to the clinic in order to finance not exceed. Also to register the names of the children that is correct.

ACHIVEMENTS

1. Transfer of funds through receiving subsidies housing, increasing school attendance, be sure to get treatment if they fall ill to join the CHF children under five years are sent to the clinic
2. Joining income generating groups to save and borrow (VICOBA). Through major challenges of beneficiaries who do not deserve they omitted on the program, of whom some of village leaders and those village leaders cancelled in the village assembly that the do not deserve to admit that they deserve.
3. Households renovations

